






# Fungua Milango. Fungua Mioyo.

Kuchunguza ukarimu wa kibiblia.


THE SALVATION ARMY

SPIRITUAL
LIFE DEVELOPMENT
INTERNATIONAL HEADQUARTERS



# Fungua Milango. Fungua Mioyo.

## Kuchunguza ukarimu wa kibiblia.

Karama, amri, tafakari ya injili.

Ukarimu sio tu ni wajibu wa wale wanaokaribisha watu ndani ya kanisa au wanaogawa vinywaji baada ya ibada. Wala sio uliowekwa akiba kwa wale wanaopewa ukarimu kama karama ya rohoni.

Sisi sote tumeitwa kutoa ukarimu kwa wale wanaotuzunguka.

Ukarimu wa kibiblia ni vitendo na mapenzi. Ni kuwapokea na kuwatumikia wengine kwa mikono yetu na mioyo yetu, na kuwakaribisha katika familia ya Mungu. Tukiwa na milango iliyofunguliwa na mioyo iliyofunguliwa, tunaweza kuwakaribisha wengine mahali watakapoonekana, wanapopendwa na pale wanapothaminiwa. Katika nafasi wanayoweza kukutana na Yesu na kugundua ukamilifu wa maisha kama Mungu alivyokusudia.

Kama wafuasi wa Yesu, tunatakiwa kusambaza mwaliko kwa kila mmoja; kwa wale tunaowafahamu na wale ambao hatuwafahamu, kwa wale wanaofanana na sisi na kwa wale wasiofanana na sisi.

Katika mfululizo huu wa siku nane, tunakualika uangalie kwa karibu mifano na hadithi za ukarimu zinazopatikana katika Biblia na uwe na muda wa kutafakari jinsi wewe unavyoweza kufanya ukarimu vizuri kwa kutumia maisha yako mwenyewe.

Kila siku utasoma kutoka katika Maandiko, na kufuatiwa na wazo fupi. Baada ya kusoma, chukua mda kutafakari au kujadili majibu yako kulingana na kile ulichokisoma, kutumia swali kutashawishi kukuongoza.

Funga kutafakari kwako kwa maombi. Mwombe Mungu akudhihirishie jambo jipya leo.



# Usumbufu.

Luka 13:10-17

Mwanamke alikuja kuabudu. Kihalisia alikuwa amepinda kiunoni. Hawezi kusimama wima. Macho yake yalikuwa kwa kudumu chini na yamekuwa hivyo kwa karibu maisha yake yote. Kama mwanamke katika jamii hii, yeye ni kipande cha mali isiyo na uwezo. Kama mwanamke aliyelemazwa na roho mwovu – amekwisha kutangazwa ana dhambi naye ni tishio kwa jamii ya dini...na bado, anakuja kuabudu. Bado hajaiacha imani yake au Mungu wake.

Yesu anamwona naye anasema – 'Tazama mwanamke.'

Tazama: Zingatia! Uwe makini!

Kwa miaka 18, watu wamemuepuka kama tauni – kwa macho yao na mguso wao – na bado, Yesu anamwona, na anamleta katikati ya jamii ya imani; anazungumza naye na kumkusanya katika kumbatio la uponyaji la Mungu. Akarejeshwa.

Yesu anapomwita 'Binti wa Ibrahimu', anampa heshima, utu na nafasi katika jamii. Ilikasirisha namna gani!

Ukarimu (siku ya Sabato!) na matokeo ya muujiza huu hayapokelewi vizuri na viongozi wa dini. Maandiko na Sheria vimegongana na upendo na ukarimu.

Unaweza kufikiria hiyo hali? Mwanamke aliyepinda anawekwa huru na anasimama wima. Mwanamke kutoka huko pembeni anapiga hatua na kuingia katikati ya sinagogi – naye anacheza!

Zungumza kuhusu usumbufu!

Kuwa mkarimu ni pamoja na kuona na kuwaita katikati wasiopendwa, walioharibika, wageni – wale walio ukingoni. Inahusu kuwafunika kwa kumbatio la joto la Mungu na kuzungumza maneno ya heshima, na ya thamani kwao. Ni hapa ambapo nguvu ya Mungu ya kubadilisha ya ukarimu inaonekana. Ni hapa ambapo uponyaji, ukamilifu na tumaini hutolewa.

Kanali Donna Evans

## Nani yuko pembeni, kwenye ukingo wa jamii yetu ya imani?

## Nani anatuhitaji tumwone, tumwite aje mbele, tumjumuishe, tumkumbatie na tumheshimu?

## Vipingamizi katika jamii yetu ya imani ni vipi vinavyozuia watu wasije kwake Yesu?

Maombi kwa siku ya leo:

Bwana, tupe macho ya kuona; moyo wa upendo wa kukumbatia na kuwajumuisha wengine; na ujasiri wa kutoa ukarimu...hata wakati ambao ukarimu husababisha usumbufu.

AMINA.



# Kumfikiria mwingine.

Mwanzo 18:6-8 Luka 10:30-37 Isaya 58:7 Wagalatia 6:10
Mathayo 10:40-42 Luka 14:12-14 I Petro 4:9

Ukarimu ni kuwafikiria wengine ambako huturuhusu sisi kumkaribisha Mungu katika hali yake,, tukionyesha upendo wetu kwa wengine. Watu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu, wakiwa na mahitaji yale yale ya kibinadamu. Tunapowaendea wengine kwa huruma na uwazi kusikiliza uzoefu wao, tutaweza kuelewa vizuri mahitaji yao.

Mgeni anaweza kuwasili akiwa amechoka, ana njaa au wakati mwingine ameumia. Kuwapumzisha kwa chakula na pumziko ni wajibu. Tunaona jibu la Ibrahimu kwa wageni wasiojulikana katika Mwanzo 18 na majibu ya Msamaria Mwema kwa mgeni aliyejeruhiwa katika mfano wa Yesu aliowashirikisha wanafunzi wake katika Luka 10. Kukaribisha na kujibu mahitaji ya wengine ni agizo maalum kutoka kwa Mungu na maelekezo aliyoyafanya Yesu kwa uwazi sana kwa wanafunzi wake wa kwanza (Mathayo 10:40-42).

Kwa utendaji, kutoa ukarimu sio kila wakati itakuwa rahisi. Lakini kama wafuasi wa Yesu, lazima tuinuke juu ya magumu yanayokabiliwa. Tunaweza tukawa wazito kufungua milango yetu na kuwakaribisha ndani wale ambao wametusababishia maumivu na kutukatisha tamaa. Wakati kusambaza ukarimu kunaonekana kuwa kugumu, tunaweza kumwita Mungu atusaidie tutimize wajibu huu, badala ya kusita kwetu abadilishe na kutupa uhakika na kuamua kwa huruma. Katika hali yetu, watu wa Kongo wana ukarimu sana sio tu kuhusu watu wa rika yao bali pia kwa wale walio maskini au wasiojiweza na kwa wageni.

Ukarimu ni tabia inayotufundisha namna ya kufungua mioyo yetu kwa wengine bila ya manung'uniko au malalamiko, kuwapokea kwa kuwajali, kuwasikiliza na kutoa malazi na chakula bila malipo.

Tunapoweka kikomo cha ukarimu wetu, tunajinyima sisi wenyewe furaha ya Mungu.

Meja Lousie Mavouna
na Kamishena Jane Paone

# Niko tayari kiasi gani kuufungua moyo wangu kwa wengine na kuwapa ukarimu kwa uhuru?

Maombi kwa ajili ya leo:

Mpendwa Baba wa Mbinguni, amsha moyo wangu kwa upendo wako ili niweze kuwakaribisha wengine katika maisha yangu, popote ninapoweza kuwa na yeyote ninayeweza kukutana naye leo.

AMINA.



# Kukubalika.

Luka 10:25-37

Ukarimu wa Kikristo huenda zaidi ya ishara rahisi za wema; huwakilisha kukubalika kimsingi kwa wengine, bila kujali historia yao, imani, au mazingira. Kukubalika hakutegemei ni kiasi gani au ni upungufu kiasi gani tunafahamu kuhusu mtu aliye mbele yetu.

Moja ya maelekezo yanayofahamika sana ya kuonyesha ukarimu yanapatikana katika Agano Jipya kitabu cha Waebrania: ' Msisahau kuwafadhili wageni, maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua' (Waebrania 13:2). Maelekezo haya sio yasiyo na msingi.

Katika Mwanzo 18, tunasoma kuhusu ukarimu mnyenyekevu wa Ibrahimu kwa wageni watatu. Ibrahimu mtu tajiri na mwenye umri, angeweza kumwita mmoja wa watumishi wake wengi awahudumie wageni hawa watatu ambao walikuwa hawafahamiki. Bali Ibrahimu kwa ukarimu aliwapa vile vizuri sana alivyokuwa navyo. Kuna mengi sana ambayo hatuyajui kuhusu wageni hawa. Ibrahimu na Sara nao hawakuwafahamu wao ni akina nani. Lakini mwitikio wao ulikuwa mwitikio wa kuwakubali kimsingi. Na, kama ilivyokuja kuonekana, walikuwa wamemkaribisha Bwana na malaika wawili.

Tunapo wakaribisha wageni, wale ambao hatuwafahamu, tunaweza bila kukusudia tukakaribisha uwepo wa mbinguni katikati yetu – ni ya ajabu namna gani!

Katika Luka 10, tunakutana na mfano wa Msamaria Mwema. Mfano huu unaonyesha jibu la kibinadamu la Msamaria kwa mgeni aliyeumizwa, jibu ambalo linapita mipaka ya kikabila na kidini.

Msamaria hakusimama akajiuliza kama huyu mgeni aliyeumizwa alikuwa ni jirani yake kabla hajamwonyesha upendo; hakufikiria ni wa taifa gani, kabila, hali, au ni msafi. Alikuwa jirani na hilo lilitosha.

Ukarimu wa kweli hauna mipaka na una utayari wa kuwakubali hata wale wanaoonekana kuwa watu wa nje. Hawapo watu wa nje kwenye upendo wa Mungu. Na hakuna sifa inayohitajika ili kupokea au kutoa ukarimu.

Meja Arif Masih

# Je, wewe hupalilia roho ya ukarimu inayotoa sura ya kukubalika bila masharti iliyoonyeshwa na Kristo?

Maombi kwa ajili ya leo:

Twaomba Bwana atupe neema ili tuendeleze ukarimu ulio ndani ya kukubalika kwa dhati, tukifuata mfano wa Kristo, aliyewakaribisha wote kwa upendo na huruma.

AMINA.


BROWN COTTAGE

# Mtiririko wa neema.

Luka 9:51-56 Luka 10:25-37 Yohana 4:1-38

Naona jinsi waandishi wa injili wanavyoelezea mwingiliano wa Yesu na Wasamaria kuwa unalazimisha bila kikomo. Bila shaka, alivyokuwa anakua huko Nazareti, inawezekana Yesu alikutana na upendeleo na ubaguzi wa jamii yake dhidi ya majirani zao. Wayahudi na Wasamaria walikuwa na malalamiko mmoja kwa mwingine yaliyotoka nyuma karne nyingi. Uhasama, tofauti za kidini na misimamo ya kisiasa iliwatenganisha na mara kadhaa iliwaka ikawa vurugu.

Inaeleza, kwamba tunapoangalia jinsi Yesu anavyochangamana na anavyozungumza kuhusu Wasamaria moja kwa moja ni kukabiliana na utamaduni: anawaadhibu wanafunzi wake kwa kukasirika wanapodharauliwa na wanakijiji Wasamaria (Luka 9:51-56); mfano wake mashuhuri una Msamaria kama shujaa na mmoja wa kuigwa (Luka 10:25-37); anakaa na kushirikishana kinywaji na mwanamke Msamaria (Yohana 4:1-38). Katika mifano hii yote, watazamaji Wayahudi wanakashfiwa. Kwetu leo, tunatakiwa kujiuliza wenyewe, Yesu alikuwa anafanya nini hapa?

Tunapomtazama Yesu na alivyojihusisha na Wasamaria kupitia kwa kioo cha ukarimu, tunaanza kuona kitu ambacho sio cha kawaida. Katika hamu yake ya kujifunua kwa mtu mwingine, anakuwa tayari kuachana na mkataba – anafanya zoezi la ukaribu na wale wasio 'wasafi', anashirikiana kwenye meza yake na 'watu wa nje' , naye anamtambua Mungu kazini ndani ya 'asiye mwamini'. Kwa sababu ya hili, maadui wanakuwa majirani, wageni wanaonekana kuwa kama zawadi, na 'mwingine' anakuwa wakala wa neema ya Mungu.

Mfano wa ukarimu wa Yesu vile vile unatuita tufungue mioyo yetu kwa njia maalum kwa ajili ya wengine, bila kujali ni akina nani. Katika kufanya hivyo, tunaweza kutarajia nafasi takatifu kujifunua inayoruhusu neema ya Mungu kutiririka kupitia kwa Roho Mtakatifu. Hapa basi, patakuwa ni mahali pa mabadiliko.

Luteni-Kanali Nick Coke

## Unaweza kufikiria kuhusu wakati wa kutoa ukarimu bila masharti kulikotoa nafasi ya neema ya Mungu kutiririka?

## Nini kilitokea?

Maombi kwa ajili ya leo:

Mpendwa Bwana, asante kutuonyesha jinsi ukarimu unavyofanana. Tusaidie tufungue mioyo yetu kwa wengine kwa njia maalum na kwa kufanya hivyo, tutengeneze nafasi kwa ajili ya neema kutiririka.

AMINA.



# Tendo la Haki.

Mambo ya Walawi 19:33-34     Mathayo 25:31-40

Ukarimu ni tendo la haki ya ufalme; ndani yake mna kumwona mwingine na mahitaji yake na kuchukua hatua ya kutaka kujibu. Sio tu aweze kuishi bali aweze kustawi na apate amani (shalom).*

Haki ya Ufalme ni kuhusu kuwakaribisha wageni kuwa sehemu ya maisha yetu na sisi tuwe sehemu ya maisha yao. Wageni, wale ambao wanaweza kuwa tofauti na sisi katika njia nyingi, wale wanaotoka nchi nyingine au waliopitia maisha tofauti, utamaduni au lugha, wanaweza kuwa wagumu kwetu kuwakaribisha. Lakini kama tunataka kufuata mfano wa Yesu na kuheshimu amri ya Mungu, tunatakiwa tuwafikie wale ambao wanaweza kujisikia hawajakaribishwa duniani kwa kumbatio lenye joto la jamii linaloweza kuonyesha upendo wa Mungu, tukitambua kwamba chochote tufanyacho kwa 'walio wadogo', tunamtendea Bwana (Mathayo 25:40). Hii inaweza kuhusisha matendo ya ukarimu wa asili kama kushirikiana chakula – lakini ni zaidi.

Katika Mambo ya Walawi 19:33–34, Mungu anatoa mwongozo mwongozo wa wazi kwamba tusiwadhulumu wageni wanaoishi katika nchi yetu, bali tuwatendee kama wenyeji, tuwapende kama tujipendavyo sisi wenyewe. Tuwape 'makazi'.

Makazi sio mahali, ni mahusiano.

Sio rahisi kuwa mgeni – bila kujua mwenendo gani ni wa kawaida, vazi lipi linakubalika au namna ya kuendesha majukumu ya maisha ya kila siku.

Kama wafuasi wa Yesu, tunatakiwa kuonyesha upendo na uvumilivu kwa mgeni aliye katikati yetu. Kwa yule anayehesabu taratibu fedha asizozizoea kwenye meza ya fedha, kwa yule mwenye mabegi mazito anayehitaji muda wa ziada kidogo apite kwenye eneo la usalama uwanja wa ndege, kwa yule anayesema maneno machache yasiyo sawa katika lugha ya kigeni. Tunatakiwa kuwakaribisha kwa upendo na kuwapa 'makazi' pamoja nasi.

Hii ni haki ya ufalme katika hali yake bora kabisa – kuishi sawa na kuweka sawa yaliyokosewa.

Kanali Wendy Swan

* 'Shalom' ni neno la Kiebrania na salaam ya Kiyahudi, mara nyingi linatafsiriwa 'amani' inaloelezea ukamilifu na haki. Maana yake ni kuungana na wengine. Na uumbaji. Na Mungu.

## Namkaribisha namna gani mgeni katikati yangu (ujirani, shuleni, katika jamii)?

## Ni kwa njia gani Mungu hujifunua kwangu kupitia kwa mgeni?

Maombi kwa ajili ya siku ya leo:

Mpendwa Bwana, tusaidie tumwone mgeni kupitia kwa macho yako. Twaomba utuonyeshe upendo na uvumilivu tunapojitahidi kujenga mahusiano nao.

AMINA.



# Kumkumbatia kila mmoja.

Luka 19:1-3

Kote katika dunia ya Jeshi la Wokovu, utamaduni wa kushirikiana kikombe cha chai ni muhimu. Nyakati hizi hutupa muda wa kupumzika, kushiriki na kupata kufahamiana. Kuchukua muda wa kufurahia chai pamoja hutengeneza nafasi ya kushirikiana. Baadaye katika kifungu hiki cha Biblia, Yesu anaomba kukaa chini mezani na Zakayo. Watu katika upana wa hadithi wakajiuliza kwanini Yesu atoe ombi kama hili. Zakayo hakuwa chaguo la kila mmoja la kuwa mwenzi kwenye 'chai'.

Watu wanaoishi na ulemavu wakati mwingine hujikuta wanaachwa wanywe chai peke yao. Rafiki yangu aligundua kwamba baada ya ibada ya Jeshi la Wokovu, watu hawakuchagua kukaa kunywa chai ya asubuhi mezani na dada yake. Dada yake wa thamani aliishi na ulemavu na hakuwa mwepesi kuelewa kila mara. Ingawa dada huyu hakutengwa kunywa chai ya asubuhi – uwepo wake kwa kweli haukukubalika. Mwana theolojia, John Swinton, anatukumbusha kwamba, 'Yesu alikaa na watu wale ambao jamii haikutaka kukaa nao.'[1]

Kuchagua nani tunakaa naye hutoa mawasiliano kwa mtu huyo na kwa dunia pana kwamba tunashukuru kwa uwepo wake na uzoefu wake wa dunia. Ukarimu mwaminifu unakubali kwamba watu wa pande zote wanaokaa kuzunguka birika la chai hudhihirisha sura ya Mungu na kuwa na karama za kushirikishana na kila mmoja. Kuchagua kukaa na mtu anayeonekana kuwa tofauti na sisi ni alama ya msingi ya mfumo wa ukarimu wa Kristo.

Coralie Bridle

[1] John Swinton, "Using Our Bodies Faithfully: Christian Friendship and the Life of Worship," Journal of Disability & Religion 19 (2015): 239.

## Unapofikiria kuhusu hali yako, ni watu gani ambao Yesu anaweza kuwa anakutaka unywe chai nao leo?

## Ni kwa njia zipi utafuatilia ukarimu mwaminifu na watu wenye ulemavu katika jamii yako?

Maombi kwa ajili ya siku ya leo:

Baba, tusaidie tuone sura ya Mungu ikidhihirishwa katika kila sura tunayokutana nayo. Tuongoze twende zaidi ya maneno ya kukaribisha na tuelekee kwenye ukarimu unaotafuta kujenga mahusiano.

AMINA.



# Kuonyesha ukarimu.

Luka 10:38-42

Mgeni katika mazingira ya Kiafriika hukaribishwa wakati wowote hata bila ya taarifa ya mapema. Methali ya Washona wa Zimbabwe, 'muenihaapedzi dura' maana yake 'mgeni hamalizi akiba yako'. Hii huangazia ukweli kwamba kuwashirikisha wengine kile ulicho nacho, pamoja na mgeni au mgeni ambaye hakukaribishwa, hakutasababisha wewe upate hasara kubwa. Methali ya Kinyarwanda, 'Umushyitsiakurishaimbuto', maana yake 'mgeni hukufanya upike mbegu ulizohifadhi kwa ajili ya kupanda'. Unapotumia rasilimali zako bora sana na zenye thamani kwa kuwatumikia wageni, wewe vile vile hupata nafasi ya kuzifurahia hizo rasilimali maalum.

Katika Luka 10:38-42, tunasoma hadithi ya Yesu nyumbani kwa Martha na Mariamu, hadithi inayozungumzia ukarimu kama unavyoeleweka katika dhana ya Kiafrika. Yesu alikuwa njiani na akaamua kuingia katika nyumba ya Martha na Mariamu bila ya mpango wa mapema, hata hivyo ukaribisho wa ukarimu bado ulitolewa. Hii inatudhihirishia kwamba ukarimu usitegemee wingi wa rasilimali zetu bali utegemee mahitaji ya wale tunaowakaribisha. Ukarimu, katika hali hii, unakwenda zaidi ya kutoa chakula tu; unaonyesha utayari wa kujali, kusaidia, kukaribisha, na kuwepo.

Katika dunia, wapo wengine ambao wana vitu zaidi vya kuwagawia wengine, lakini bado hawako tayari kuachana na vile walivyo navyo. Wapo wengine ambao wana vitu vya kutosha tu lakini wanapata shida kuwaalika wengine waje washirikishane. Iwe tuna ghala imejaa rasilimali, tuna kidogo tu kilichobakia kabatini, tunaitwa tufungue milango yetu na tuwakaribishe wageni kwa njia yoyote. Yesu anatuita tuwepo kutumika, hata wakati tukijisikia hatujajiandaa au tuna rasilimali kidogo. Anatutaka tutoe kwa wengine wakati kuna hitaji, sio tu wakati inawezekana au inapotupendeza sisi.

Ukarimu wa kweli unatokea kwenye moyo mkarimu na upendo unaojali unaotaka mema kwa wote, pamoja na kwa wageni.

Luteni Kanali Celestin Ayabagabo
na Kanali Bishow Samhika

# Kutafakari hadithi hii fupi, nini huhamasisha matendo yako ya ukarimu leo?

# Je, ukarimu wako hudhihirisha utayari wako, na uwepo wako kuwatumikia wengine bila ya mipaka?

Maombi kwa ajili ya leo:

Mpendwa Bwana, ninapowafikiria wale ambao wanaweza kuonekana mlangoni kwangu bila taarifa, nisaidie kuwaonyesha aina ya ukarimu ambao unatoka moyoni...unaosambaza upendo na kujali na wa hamu ya kuwakaribisha kama dhihirisho la upendo na neema yako isiyo na mipaka.

AMINA.



# Mtindo wa maisha.

Warumi12:9-21 Luka 10: 38-42 Matendo 18:2-3
Mwanzo 18:1-8 Matendo 9:36 Ruthu 2:8-16

Mungu huwajali watu wake kupitia kwa watu wake.

Katika mfululizo huu, tumetafakari mifano kadhaa ya ukarimu iliyopatikana ndani ya Biblia na mwito wa kusambaza ukarimu bila ya manung'uniko na kwa ukarimu, sio tu kwa wageni wetu bali vile vile kwa watakatifu na kwa watu tusiowajua.

Kama waamini na sehemu ya Mwili wa Kristo, tunadhihirisha kufanana na Kristo na upendo wa Mungu tunapotoa ukarimu. Fikiria kuhusu dunia ambayo sisi sote tumejitoa kufungua milango yetu, kuwaheshimu wengine kuliko sisi wenyewe na kushirikishana mmoja na mwingine!

Ukarimu ni zaidi ya zoezi la nyakati fulani, ni njia ya kuishi. Warumi 12:9-21 inafafanua sifa za ukarimu wa Kikristo. Unahitaji muda wetu, fedha, ujuzi na rasilimali nyingine tushirikishane na wengine kwa wema na kwa heshima. Unadai kujitoa sadaka. Ni upendo katika matendo.

Maandiko yanatwambia kwamba Yesu, wanafunzi wake na manabii walikaribishwa katika nyumba nyingi kwa upendo, heshima na kwa wema wa zaidi ya kawaida.

Martha na Mariamu walitoa ukarimu kwa Yesu (Luka 10:38-42). Prisila na Akila walimkaribisha Paulo (Matendo 18:2-3).

Sara na Ibrahimu walionyesha ukarimu kwa wageni wao (Mwanzo 18:1-8). Tabitha alionyesha wema kupitia kwa matendo yake (Matendo 9:36), na Boazi alionyesha ukarimu wa kipekee na wema kwa Ruthu (Ruthu 2:8-16). Orodha inaendelea.

Biblia ndiyo msingi wa maisha ya Kikristo, na kutokana na wingi wa mifano tunayoshirikishwa katika Neno la Mungu, tunaweza kujifunza kwamba kufanya ukarimu maana yake ni kuwakubali watu, kushirikishana nao, kukabiliana na mahitaji yao sawa na huruma ya Mungu, na kuwatendea kwa heshima.

Tunamtukuza Mungu kwa ajili ya Jeshi la Wokovu (Kanisa), wanaotenda ukarimu kwa mikono ya ukarimu kati ya wale wenye uhitaji, jamii zinazoteseka na wakimbizi. Na yote ni kuleta utukufu, heshima na sifa kwa Mungu ili watu wafahamu neema iokoayo ya Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Hili lazima liwe ndilo lengo letu la mwisho.

Mtu binafsi anaweza kuuishi ukarimu na wengine katika familia zetu, sehemu za kazi na katika jamii, na bila shaka Kanisani. Lakini hebu tusijaribu kamwe kufanya hivyo sisi wenyewe. Tumtegemee Mungu, Mwanae Yesu Kristo na uwezo wa Roho Mtakatifu tunavyofungua milango yetu na mioyo yetu kwa wengine kwa upendo.

Captain Dorothy Macwan

# Je, sisi kwa kweli tunatenda ukarimu kwa upendo, huruma, na kwa ukarimu, au tunapitia tu katika mwendo bila ya makusudi ya moyoni?

Maombi kwa ajili ya leo:

Mpendwa Baba wa Mbinguni, katika huruma na upendo wako, twaomba tutoe ukarimu kwa wote, kwa utukufu na heshima yako na kwa kusudi la Ufalme wako, katika uwezo wa Roho Mtakatifu. Katika Jina la Yesu.

AMINA.

SPIRITUAL
LIFE DEVELOPMENT
INTERNATIONAL HEADQUARTERS

Tunalishukuru Baraza la Kimataifa la Theolojia kwa kazi waliyoifanya kuhusu somo la ukarimu kibiblia kwa maandalizi ya mtiririko huu.
Pata zaidi kuhusu wachangiaji wetu na kuhusu wajibu na kazi ya Baraza la Kimataifa la Theolojia kwenye salvationarmy.org
All images sourced from pexels.com. For queries, please contact ihq-sld@salvationarmy.org